BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

# BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Pili – Tarehe 12 Septemba, 2024**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023/2024.

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023/2024.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi juu ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023/2024.

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais juu ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

48. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Ni miradi ipi ya kijasiriamali ambayo wahitimu wa matumizi ya dawa za kulevya ikiwemo 'methadone' wamewezeshwa.

### Ofisi ya Rais, Ikulu:

245. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:

Hivi karibuni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) ilitoa kauli katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha hadhi maalumu kwa 'Diaspora' wenye asili ya Tanzania ili kuwawezesha kuchangia miradi ya maendeleo nchini Tanzania. Utekelezaji huu unakuja ikiwa ni pamoja na kuzifanyia marekebisho baadhi ya sheria zake.

(a) Je, Serikali imejiandaa vipi na mabadiliko haya.

(b) Je, Serikali ina chombo chochote kinachosajili 'Diaspora' wenye asili ya Zanzibar na kwa takwimu ni Diaspora wangapi walio na asili ya Zanzibar waliopo ughaibuni.

(c) Kwa kuwa utekelezaji wa hadhi maalumu unahitaji marekebisho ya baadhi ya sheria, Je, ni lini Serikali italeta miswada ya sheria kwa ajili ya marekebisho ya baadhi ya sheria ili kuruhusu utekelezaji wa hadhi maalumu za 'Diaspora' wa Zanzibar.

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

108. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Bila ya shaka yoyote Wizara yako inafanya tathmini ya kuongezeka na kupungua kwa vitendo vya rushwa ya ngono kwa kila mwaka, kama ilivyofanya kwa kipindi cha mwaka 2020 - 2023.

(a) Watuhumiwa wangapi wamepatikana na hatia za rushwa

za ngono katika maeneo ya uongozi, ajira, elimu na makosa ya usalama barabarani.

(b) Rushwa ya aina gani kwa sasa imekithiri mno.

(c) Kwa kiasi gani rushwa ya ngono katika ngazi za vyuo vikuu inaathiri ubora wa elimu na kwa namna gani inadhibitiwa.

## Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

238. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa muda mrefu sasa eneo la barabara ya kutokea Kisiwandui kuelekea Michenzani limekuwa na msongamano mkubwa wa gari na kuleta usumbufu kwa watumiaji wengine wa barabara.

(a) Je, kuna mpango gani wa kuiondoa kadhia hiyo.

(b) Kwa kuwa katika eneo hilo lipo kituo cha gari za abiria, Je, kuna mpango gani wa kuweka mazingira mazuri ili kituo hicho kisiwe kero barabarani.

## Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

229. MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Pongezi kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuuboresha Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Pamoja na maboresho hayo, bado kuna changamoto kubwa inayowakabili wananchi katika kupata mikopo hiyo.

(a) Je, vipi Serikali inalifahamu tatizo hili.

(b) Je, ni mkakati gani utakaotumika kuitatua changamoto hiyo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

57. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa nini ligi kuu ya Zanzibar inapoteza mwamko, hamasa na vuguvugu kutoka kwa mashabiki wengi wanaohudhuria viwanjani licha ya udhamini mnono kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

61. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

(a) Ni lini Wizara yako ilikaa na kusikiliza changamoto za wabunifu mbali mbali nchini na ni yepi matokeo chanya ya kikao hicho.

(b) Sababu gani zinazopelekea kazi mbali mbali za wabunifu nchini kwetu kutokuwa na muendelezo mzuri.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

5. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tunaipongeza Serikali kwa maamuzi ya kuwataka wanafunzi wanaochukuwa ujauzito kuendelea na masomo baada ya kujifungua.

(a) Ni ipi takwimu halisi ya wanafunzi hao kwa sasa.

(b) Ni upi wajibu wa wazazi na walimu katika kuhakikisha wanafunzi hao wanarudi shuleni baada ya kujifungua.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

62. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Wananchi wa jimbo la Mwanakwerekwe wanampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendeleza miradi mbali mbali jimboni humo, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa skuli za kisasa za ghorofa, ujenzi wa soko la kisasa la Mwanakwerekwe, ujenzi wa barabara za

ndani kwa kiwango cha lami pamoja na kujenga hospitali ya Wilaya.

Je, ni kwa kiasi gani wananchi wa jimbo la Mwanakwerekwe watafaidika na upatikanaji wa ajira zisizo za kitaalamu kutokana na ujenzi wa mradi wa *flyover* na ule wa kituo cha maegesho ya magari cha kisasa kinachotarajiwa kujengwa kwenye bwawa la Mwanakwerekwe.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

241. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Je, Serikali ina mipango gani ya kurekebisha sheria zake ili kuwawezesha wawekezaji binafsi katika miradi ya umeme Zanzibar.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Ripoti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023/2024.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Ripoti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**12 Septemba, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**